AFRICAN UNION
الاتحاد الأفريقي
UMOJA WA AFRIKA

UNION AFRICAINE
UNIÃO AFRICANA
UNIÓN AFRICANA

Addis Ababa, Ethiopia S.L.P 3243 Simu: +251 115 517 700 Nukushi : +251 115 517 844
Tuvuti : www.au.int

MKUTANO MKUU WA UMOJA WA AFRIKA
Mkutano wa Kawaida wa Thelathini na Saba
17 - 18 Februari 2024
Addis Ababa, ETHIOPIA

Assembly/AU/23(XXXVII)
Matini chanzi: Kiingereza

TOLEO LA TATU LA JUKWAA LA AFRIKA LA UTAMADUNI WA AMANI & WA KUTOKUWA NA UKATILI "BIENNALE OF LUANDA",
(*Kipengele Kilipendekezwa na Jamhuri ya Angola)*

Rua Major Kanhangulo, nº 37, Edifício Sede do MIREX,
Rés-do-chão, Bairro Ingombota (Mutamba), Luanda-Angola
Telf. + 244 226 430 510 | E-mail: direccao.africa@mirex.gov.ao

GOVERNO DE ANGOLA | mirex.gov.ao Ministério das Relações Exteriores

REPÚBLICA DE ANGOLA

MUHTASARI WA RIPOTI YA KONGAMANO LA 3 LA UMAJUMUI KWAAJILI YA UTAMADUNI WA AMANI NA KUTOKOMEZA UKATILI – "LINALOFANYIKA KILA BAADA YA MIAKA MIWILI LA LUANDA"

ITAKAYOWASILISHWA WAKATI WA BARAZA KUU NA MKUTANO MKUU WA WAKUU WA NCHI NA SERIKALI WA UMOJA WA AFRIKA, ULIOPANGWA KUFANYIKA MJINI ADDIS ABABA KUANZIA TAREHE 14 HADI TAREHE 18 FEBRUARI 2024.

I. UTANGULIZI

1. Waraka huu unajumuisha ripoti ya muhtasari wa Toleo la 3 la Kongamano la Umajumui la Utamaduni wa Amani na Utulivu – Linalofanyika kila baada ya miaka miwili laLuanda, lililofanyika katika mji mkuu wa Jamhuri ya Angola, Luanda, tarehe 22, 23 na 24 Novemba 2023, chini ya kauli mbiu "**Elimu, Utamaduni wa Amani na Umajumui kama nyenzo za Maendeleo Endelevu ya Bara la Afrika**".

2. Kongamano linalofanyika kila baada ya Miaka Miwili la Luanda ni matokeo ya Uamuzi wa 558/XXIV, uliopitishwa katika Kikao cha 24 cha Mkutano Mkuu wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika, uliofanyika Januari 2015, ambao uliagiza Kamisheni ya Umoja wa Afrika "kuchukua kila hatua inayofaa, kwa kushauriana na UNESCO na Serikali ya Jamhuri ya Angola, kwa ajili ya kuandaa Kongamano la Umajumui kwaajili ya Utamaduni wa Amani linalofanyika kila baada ya miaka miwili la Luanda ", sambamba na Mpango wa Utekelezaji wa Utamaduni wa Amani Barani Afrika.

3. Kongamano linalofanyika kila baada ya miaka miwili la Luanda linatoa jukwaa pana la kutafakari na kukuza malengo, miradi, maono, kanuni na maadili, likiwaleta pamoja Wakuu wa Nchi na Serikali, viongozi vijana, mashirika ya kimataifa, taasisi za fedha, sekta binafsi, asasi za kiraia, jumuiya za kisayansi, sanaa na michezo, kushughulikia, kusambaza mawazo na kuhamasisha juhudi binafsi na za pamoja na ya kielelezo na endelevu kwa ajili ya amani barani Afrika na duniani.

II. MADHUMUNI YA TOLEO LA TATU LA KONGAMANO

4. Toleo la Tatu la Kongamano linalofanyika kila baada ya miaka miwili la Luanda lilikuwa na madhumuni yafuatayo :

(i) Kuimarisha ushirikiano wa kubadilishana maono kuhusu utamaduni wa amani, usalama, umajumui, demokrasia barani Afrika, pamoja na kujenga jamii zenye amani zaidi, kubadilishana mitazamo katika nyanja za kisiasa, kiuchumi na kijamii, ili kuimarisha mihimili ya maendeleo muhimu ya bara hili;

(ii) Kuthibitisha dhamira ya Angola ya kushirikiana na Umoja wa Afrika katika mchakato wa kuandaa na kutekeleza shughuli zinazohusu amani na utulivu barani Afrika, ndani ya mfumo wa Ajenda ya Rais wa Jamhuri ya Angola naKinara wa Amani na Maridhiano wa Umoja wa Afrika barani Afrika, João Manuel Gonçalves Lourenço ;

(iii) Kushirikiana na UNESCO katika kuandaa Mipango Kazi ya kukuza elimu, sayansi na usambazaji wa sanaa kwa ajili ya kukuza Utamaduni wa Amani na Utulivu ;

(iv) Kuhimiza tafakuri juu ya faida za utekelezaji wa elimu bora, umajumui, ushirikiano wa bara, hatua za kudhibiti tabianchi , matumizi ya nishati mbadala na teknolojia ya habari na mawasiliano, uwezeshaji wa wanawake na wasichana, pamoja na uimarishaji wa utawala wa kidemokrasia na utawala wa sheria barani Afrika.

III. MUUNDO WA MDAHALO

5. Toleo la 3 la Kongamano lifanyikalo mara mbili kwa mwaka la Luanda lilifanyika katika umbizo la mseto, wageni walishiriki ana kwa ana na kwa njia ya mtandao katika Majopo 6 ya Mdahalo , na lilikuwa na muundo ufuatao:

a) Sherehe ya Ufunguzi;
b) Mazungumzo ya vizazi kati ya Wakuu na vijana;
c) Makongamano ;
d) Taarifa ya mwisho na
e) Kutembelea majengo ya kale ya utamaduni

6. Kati ya mada 6 zilizoshughulikiwa, zifuatazo zinajitokeza**:**

a) Mazungumzo kati ya Wakuu wa Nchi na Vijana kutoka nchi mbalimbali za Afrika, chini ya Jopo la "Vijana, Watendaji katika Kukuza Utamaduni wa Amani na Mabadiliko ya Kijamii Barani Afrika";

b) "Wajibu wa Wanawake katika Amani, Usalama na Mchakato wa Maendeleo" na

c) "Changamoto za Kimaadili za Mabadiliko ya Tabianchi: athari, marekebisho na udhaifu".

IV. TAASISI ZILIZOSHIRIKI

7. Kongamano hilo lilihudhuriwa na wageni 790, wakiwemo waandaaji pamoja na wazungumzaji, na taasisi zifuatavyo hasa:

(1) Rais wa Jamhuri ya Angola
(2) Rais wa Shirikisho la Jamhuri ya Kidemokrasia ya Ethiopia
(3) Rais wa Jamhuri ya São Tomé na Príncipe

(4) Rais wa Jamhuri ya Cape Verde
(5) Rais wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika
(6) Naibu Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO
(7) Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Angola
(8) Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Namibia
(9) Waziri Mkuu wa Equatorial Guinea
(10) Rais wa zamani wa Nigeria
(11) Rais wa zamani wa Msumbiji
(12) Rais wa zamani wa Malawi
(13) Rais wa zamani wa Afrika Kusini
(14) Katibu Mkuu wa Baraza la Makanisa ya Kikristo nchini Angola.

V. NAFASI YA VYOMBO VYA MAANDALIZI

a) UMOJA WA AFRIKA

8. Toleo la 3 la Kongamano linalofanyika kila baada ya Miaka Miwili la Luanda lilifanyika katika ngazi ya Bara la Afrika, na kuchangia katika utekelezaji wa Matarajio ya Ajenda 2063 ya Umoja wa Afrika na, hasa, kampeni ya "Kupigania Amani" na mradi kabambe wa "Kutokomeza vita ifikapo mwaka 2030".

9. Vilevile, AU ilikuwa na jukumu la kuhamasisha vyombo vingine vya AU na Jumuiya za Uchumi za Kikanda, kutekeleza programu na miradi inayotolewa na jukwaa, kuratibu vikao vya mashauriano na washirika wa kitaasisi wa AU ili kuwa na maono ya pamoja, malengo na matokeo, pamoja na kuratibu mazungumzo kati ya vizazi, kwa kushirikiana na Serikali ya Angola na UNESCO, na kuandaa na kufanya makongamano.

b) UNESCO

10. UNESCO ilichangia moja kwa moja katika kukuza dira, malengo na matokeo yanayotarajiwa ya toleo la 3 la Kongamano linalofanyika kila baada ya miaka miwili la Luanda, kuhakikisha mashauriano na uratibu unaoendelea kati ya Serikali ya Angola na AU katika kuandaa midahalo na mazungumzo kati ya vizazi.

11. UNESCO pia ilitoa msaada wa kiufundi katika kuandaa hati, taarifa kwa vyombo vya habari, muhtasari kwa wazungumzaji na kutangaza Kongamano la kila baada ya Miaka miwili la Luanda kwenye tovuti, mitandao ya kijamii na vyombo vya habari vya kimataifa.

c) SERIKALI YA ANGOLA

12. Kwa ushirikiano muhimu wa AU na UNESCO katika kufanya Kongamano hilo, Jamhuri ya Angola ilihakikisha panakuwepo lojistiki husika, uhamasishaji, usalama, usafiri, kuwasili na kuondoka kwa wageni, malazi na mafanikio ya ushiriki wa wote, kuhakikisha mahudhurio ya kuridhisha ya wageni 790 wa kitaifa na kimataifa katika ukumbi wa hafla hiyo, ambapo midahalo yake ilirushwa mubashara na vyombo vya habari vya Angola na kimataifa.

13. Jamhuri ya Angola, AU na UNESCO walitayarisha Taarifa ya Mwisho ya toleo la 3 la Kongamano linalofanyika kila baada ya Miaka miwili la Luanda.

VI. MATOKEO YALIYOPATIKANA

14. Toleo la 3 la Kongamano lifanyikalo kila baada ya Miaka miwili la Luanda lilikuwa na matokeo yafuatayo:

(i) Kuongezeka kwa ushirikishwaji wa maono ya amani na demokrasia barani Afrika; utekelezaji wa kubadilishana maarifa na kuimarisha uwezo; kuimarisha mipango ya uwekezaji, uhifadhi na udhibiti wa sanaa, sayansi, elimu na utamaduni kwa ajili ya amani na kuongeza uelewa kuhusu heshima ya utambulisho wa kitamaduni na uanuwai;

(ii) Ukuzaji wa dira jumuishi ya historia na urithi wa Kiafrika, kukuza kanuni za kitamaduni, utambulisho na ufufuaji wa maadili ya Kiafrika; kuongeza uelewa kuhusu athari za mabadiliko ya tabianchi kuhusiana na amani na usalama na kuimarisha dhamana ya vijana katika kuchangia utatuzi wa migogoro na mafanikio ya maendeleo;

(iii) Kuimarishwa mapambano dhidi ya propaganda na masimulizi yanayoungwa mkono na makundi jeuri na yenye itikadi kali, kuhimiza utayari wa bara la Afrika katika kukomesha vurugu na matumizi ya nguvu kinyume cha sheria, kuheshimu amani, taasisi zilizochaguliwa kidemokrasia, uhuru wa watu na bidhaa kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine na umoja wa kieneo; utendaji wa kawaida wa taasisi, haki na utu wa binadamu.

VII. HITIMISHO LA TOLEO LA 3

15. Miongoni mwa mahitimisho na mapendekezo mengi muhimu yaliyotokana na toleo la 3 la Kongamano la kila baada ya miaka miwili la Luanda, tungependa kuangazia yafuatayo:

(i) Washiriki walimpongeza Rais wa Jamhuri ya Angola, João Manuel Gonçalves Lourenço, kwa Kongamano hilo kufanyika kwa mafanikio, na kumhimiza Rais kufanyia kazi toleo la 4 la Kongamano linalofanyika kila baada ya Miaka Miwili la Luanda mnamo 2025, kama nafasi ya kutafakari, mazungumzo kati ya Wakuu wa Nchi, vijana, viongozi wa taasisi, wanazuoni na wanasiasa kuhusu masuala ya Afrika, kama vile kunufaika na idadi ya watu na kutimiza Ajenda 2063 na Malengo ya Maendeleo Endelevu .

(ii) Jukwaa lilizitaka nchi wanachama wa AU kuendelea kudumisha hatua za utekelezaji zaidi wa Mkataba wa Vijana wa Afrika, kukomesha vita , kukuza umajumui , maridhiano na umoja, kama sababu za maendeleo ya watu wa Afrika, na pia ilipendekeza Angola ishirikiane na UNESCO kuandaa Mipango ya Utekelezaji kwa ajili ya kukuza elimu, sayansi, na usambazaji wa sanaa ili kukuza Utamaduni wa Amani.

(iii) AU, UNESCO na Jamhuri ya Angola zimejitolea kuendeleza hatua zinazolenga kuongeza ufahamu na heshima kwa utambulisho wa kitamaduni na anuwai, kuwashirikisha washirika wengine wa kijamii katika kukuza maono jumuishi ya historia na urithi wa Afrika na kukuza desturi za kitamaduni, utambulisho na ufufuaji wa maadili ya Kiafrika, pamoja na kuendeleza hatua za uelewa wa bara na kimataifa juu ya athari za mabadiliko ya tabianchi kuhusiana na amani na usalama.

(iv) Washiriki walipendekeza kujumuishwa kwa Kongamano la Umajumui la Utamaduni wa Amani na Utulivu "Jukwaa linalofanyika kila baada ya miaka miwili la Luanda" katika Ajenda ya kudumu ya Umoja wa Afrika, pia kubainisha mwezi mahususi ambapo matoleo yajayo ya Jukwaa hilo yatafanyika kuanzia sasa.

(v) Washiriki wa hafla hiyo walikaribisha mpango wa Baraza la Makanisa ya Kikristo nchini Angola kuhimiza mkutano wa kiekumene kuhusu urejeshaji wa tunu za kimaadili na kiraia katika jamii, kama sehemu ya shughuli sambamba na toleo la 3 la Kongamano linalofanyika kila baada ya Miaka Miwili la Luanda.

WIZARA YA MAMBO YA NJE, LUANDA, ANGOLA, DISEMBA 7, 2023.-

AFRICAN UNION UNION AFRICAINE

African Union Common Repository **http://archives.au.int**

Organs Assembly Collection

2024-02-17

3RD Edition of the Pan-African Forum for the Culture of Peace & Non-Violence “Biennale of Luanda”, (Item proposed by the Republic of Angola

African Union

African Union

https://archives.au.int/handle/123456789/10574

Downloaded from African Union Common Repository